JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/74, Fax: +255222129878,
General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

Serikali imeunganisha Taasisi 72 katika Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali ('Government Communication Network-GovNet) kupitia Mkongo wa Taifa (NICTBB) kwa Optic Fiber Cable. Pia Taasisi 77 zilizo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI zitaunganishwa kwenye mtandao huo kufikia Disemba 2016. Taasisi hizo pia zimefungiwa Mtandao wa Ndani wa Mawasiliano (LAN) pamoja na mfumo wa simu zenye itifaki ya intaneti (Internet Protocol Phones (IP phones) Private Branch Exchange (IP PBX).

Taasisi 72 ni pamoja na Wizara zote, Idara Zinazojitegemea (Ofisi ya Bunge, NAOT) na Wakala za Serikali (TBA, WMA, BRELA). Taasisi 77 kutoka mikoa 20 ya Tanzania Bara (Dodoma, Tanga, Dar es Salaam, Kagera, Lindi) Kila mkoa unajumuisha ofisi ya Mkuu wa Mkoa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji.

Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutaipunguzia Serikali gharama za mawasiliano zilizokuwa zinatolewa, kutasaidia taasisi kuwa na mawasiliano bora ya kielektoni (data, sauti na video), kutaongeza kasi ya masafa ya intaneti ,kutawezesha matumizi ya mifumo shirikishi ya TEHAMA, kutaboresha utendaji kazi na kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa umma.

Aidha, taasisi zilizounganishwa na mfumo wa simu zenye itifaki ya intaneti (Internet Protocol) ambazo hufanya kazi kwa ufanisi zitaweza kuwasiliana taasisi baina ya taasisi kwa urahisi. Kwa mfano, mtumishi wa taasisi moja katika taasisi hizo anaweza kupiga simu kwenda taasisi nyingine ya nje ikawa kama umepiga simu ya 'extension' ndani ya ofisi moja. Pia taasisi zinaweza kufanya mikutano kwa njia ya simu (teleconference). Orodha ya namba hizo inapatikana katika tovuti ya Wakala www.ega.go.tz

Ili kufanikisha zoezi hilo, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wakala imetoa Mafunzo kwa taasisi tajwa hapo juu, kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Mtandao wa Serikali na matumizi ya simu zinazotumia itifaki (IP Phones) kwa Wataalamu wa TEHAMA na Makatibu Muhtasi kutoka Wizara, Taasisi Zinazojitegemea, Wakala za Serikali zilizounganishwa.

Mpango wa Serikali ni kuzifikia mikoa na halmashauri zote hapa nchini ili kutumia mawasiliano ya simu za itifaki, barua pepe na mifumo ya TEHAMA katika kubadilishana taarifa.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx xxx**MWISHO**xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

Imetolewa Na:
SUZAN MSHAKANGOTO
MENEJA WA HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO (eGA)